

Maswali

1. Daudi alipomuona Bath-sheba alikuwa wapi?
2. Mme wa Bath-sheba alikuwa mwana jeshi, aliiitwa nani?
3. Alifanyiwa nini kwa kufuata matakwa ya mfalme Daudi?
4. Mungu alimwambia Daudi eti nini itafanyika kwake kwa ajili ya kukosa?
5. Nini ilifanyika kwa mtoto wa kwanza wa Bath-sheba na Daudi?
6. Nani alimuwa Amnoni mwana wa Daudi kwa kitendo alichofanya kwa dadake?
7. Daudi na Bath-sheba walipata mtoto mwingine, aliiitwa nani?
8. Daudi alikufa akiwa na miaka 70. Alitawala kwa mda gani?
9. Nani alikuwa mfalme baada ya Daudi kufa?

Majibu

1. Kwa dari la jumba la mfalme.
2. Uria.
3. Aliwekwa mbele ya jeshi na akauwawa.
4. Mungu alisema ataadhibu nyumba ya Daudi.
5. Alikufa.
6. Absalomu.
7. Sulemani.
8. Alitawala kwa miaka 40.
9. Sulemani

SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 1 Mwaka wa 2



18 Daudi na Bathsheba

Marejeo

2 Samweli 11


Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba zote huwa tunakosa lakini tukiomba Mungu msamaha wa kweli, hutusameha.

Maneno maalum

1. Daudi + Kosa (dhambi).
2. Bath-sheba + Yoabu + Uria auwawa.
3. Mungu akasirika + Nathani + Daudi atubu + adhabu ya Mungu.
4. Wana wanne wakafa + shida za familia.
5. Sulemani.
6. Sulemani atiwa mafuta na Sadoki + Daudi akufa.

18.1 Daudi alipokuwa mzee alifanya kosa. Alijua ni makosa kuchukua kitu cha mtu, lakini jioni moja alipokuwa ako kwa dari ya jumba ya mfalme, aliangalia chini na akaona mwanamke mzuri. Jina lake alikuwa Bath-sheba na mmewe alikuwa mmoja wa askari wa Daudi, jina lake Uria. Daudi alimpenda Bath-sheba.



18.2 Daudi alimtaka Bath-sheba sana na kutuma wajumbe wake wamlete kwa jumba la mfalme. Uria hakukuweko. Alikuwa ameenda vitani, Daudi alilala na Bath-sheba na baadaye akaambiwa alikuwa anaenda kupata mtoto. Daudi alisumbuliwa kwa sababu alijua amekosa. Alituma habari kwa Yoabu mkuu wa jeshi amuweke Uria mbele ya vita ili auwawe. Baada ya Uria kufa, Daudi alimuoa Bath-sheba.

18.3 Mungu alimkasirikia Daudi sana na akatuma mtumishi wake Nathani amwambie kuhusu hiyo dhambi. Daudi alisikitika sana, kwa hivyo Mungu hakumuua lakini akamwambia, "Kwa sababu umefanya haya makosa, utakuwa na shida nyingi kwa nyumba yako." Na ni kweli Daudi alikuwa na shida nyingi sana.

18.4 Alikuwa na shida nyingi kwa familia. Alifiwa na wana wake wanne. Kwanza mtoto aliyezaliwa na Bath-sheba alikufa mchanga. Pili, mzaliwa wake wa kwanza Amnoni alimnazisi binti wake Tamari. Absalomu mwana wake mwingine aliudhika na hicho kitendo na akamuwa Amnoni. Tatu, Absalomu alikubaliwa na watu wengi awe mfalme badala ya Daudi. Daudi alipigana, akashinda na Absolomu akauwawa. Hatimae mwana wake wa nne Adonija aliuwawa kwa sababu yeye naye alitaka kuwa mfalme. Kwa hivyo yote aliyoysema Mungu yalitendeka, wana wa Daudi wanne walikufa.

18.5 Baadaye Bath-sheba alizaa mwana mwingine aliyeitwa Sulemani. Ingawaje Sulemani hakukuwa mwana wa kwanza wa Daudi, alimchagua awe mfalme baada yake.

18.6 Daudi alipokuwa mzee, aliambia Sadoki amminie mafuta kichwani kuonyesha kwamba yeye ndiye atakuwa mfalme. Baadaye Daudi akafa na umri wa miaka 70. Alikuwa ametawala kwa miaka 40. Baada ya kifo cha Daudi, Sulemani alikuwa mfalme wa Israeli.

